



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.S.20/86/Vol.II/42

04.08.2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kuomba nafasi ya Ajira za Watendaji wa Vijiji na Madereva kwa masharti ya kudumu. Tangazo hili ni baada ya kupokea vibali vya ajira mbadala vyenye Kumb.Na. FA.170/371/O1"A"/188 cha tarehe 4 Julai, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mchanganuo wa nafasi hizo ni kama ufuatao: -

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III - Nafasi 5

(a) KAZI NA MAJUKUMU

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao kwa kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa Vikao vya Wataalamu katika ngazi ya Kijiji.
- x. Kupokea na kutatua matatizo / malalamiko ya wananchi
- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
- xii. Kuwajibika kwa Mtendaji wa Kata.

(b) SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na Cheti cha Kidato cha Nne (IV) / Sita (VI)
- ii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada / Cheti ambayo ni NTA (Level 5) katika moja ya fani zifuatazo: - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Rasilimali Watu, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

(c) Ngazi ya Mshahara

TGS. B1 :

2. DEREVA II - Nafasi 05

(a) KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iii. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- iv. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- v. Kufanya usafi wa gari
- vi. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.

(b) SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na Cheti cha kuhitimu Kidato cha Nne (IV)
- ii. Awe na Leseni daraja "C" au E ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha VETA au NIT au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

(c) Ngazi ya Mshahara

TGS. B1 :

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE AMBAYO
NI LAZIMA KUZINGATIA**

- (a) Mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania
- (b) Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya Jinai
- (c) Awe hajawahi kufukuzwa au kupunguzwa kazi Serikalini
- (d) Maombi ni lazima yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, kuhitimu Elimu ya Sekondari (*Result Slips hazitakubaliwa*) na vyuo vya mafunzo au Taaluma.
- (e) Maombi ni lazima yaambatanishwe na picha mbili za "passport size" za hivi karibuni
- (f) Maombi ni lazima yaambatishwe na wasifu "Curriculum Vitae" zenye mawasiliano ya uhakika, Anuani, barua pepe na namba za simu.
- (g) Awe na Umri wa miaka 18 na usiozidi miaka 45
- (h) Mwombaji awe hajawahi kuajiriwa Serikalini na kupata cheki namba.
- (i) Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na cheti cha taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi wa Taifa (NACTE)
- (j) Awe na kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba ya NIDA


Waombaji wote wenye sifa watume maombi yao kwenye anwani ifuatazo: -

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Meru,
S. L. P 462,
USA - RIVER.**

Barua za maombi zitapokelewa kuanzia tarehe 09.08.2023 hadi tarehe 22.08.2023 saa 9.30 Alasiri.

Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya www.merudc.go.tz na mbao za matangazo katika Ofisi ya Makao Makuu ya Halmashauri na Ofisi za Vijiji na Kata zilizopo Halmashauri ya Meru.

Tangazo hili limetolewa na:


**Mwl. Zainabu J. Makwinya
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**

